

Shairi lifuatalo liliandikwa na Hassan Adam wa Cologne Ujerumani kwa Rafiki yake Bakari alipokuwa anataka kufunga ndoa, ambayo ilikuwa inajitomeka katika mila na desturi za Kijerumani badala ya zile asilia za Kiafrika au za Kitanzania, kwa Penzi lake Bakari ambalo lilipevuka na kuvuka mipaka yote ya Kidini, utamaduni na mila za Kitanzania, Je unakubaliana na Wosia wa Mshairi Hassan Adam au kwa jina lingine HAU? endelea kusoma...!

WOSIA

1. Muadham ndugu Bakari, nina yangu leo nia.
Ya kukujavya khabari, zilizo na welekea.
Kwani maisha bahari, kila mtu kuzamia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
2. Allah Allah jihadhari, uzunguni kuzamia.
Tena epuka khatari, kuoa wa Almaniam.
Zisikukumbe kikiri, utanza kujutia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
3. Nisemayo tafakari, yapate kukuingia.
Unayo yako khiyari, kukataa kiamua.
Ni wengi walihakiri, ndipo wakaumia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
4. Ukimuoa kwa siri, ndugu bila kubalia.
Ukaona ni fakhari, kuoa wa Amerkia.
Mno utahisi hari, mke kwenu kuingia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
5. Hutakuwa na khiyari, ukioa Jarmania.
Hajali yeye nadhari, kila siku maudhia.
Atataka lake gari, hali wewe watembea.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
6. Kila siku ni safari, shamba hatapalilia.
Atasikiza santuri, jikoni hataingia.
Mitaani hunawiri, raha itakuishia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
7. Sikuzote kubwa shari, kitanda hutalalia.
Zake nyingi ni jeuri, utadhani baharia.
Itavimba kapilari, hasira kukuingia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
8. Kotekote mwasanjari, maduka kuyaingia,
Mkitafuta sukari, mengi kumtimizia,
Mauaye na shajari, apate kufurahia,
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
9. Mbele ya akhiyari, lake atang'ang'ania.
Nyingi atatoa amri, kamwoshee sufuria.
Na biya ya bilauri, mezani kumwekea.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
10. Hapiki mke futari, ilivyo kama sheria.
Atachukia ambari, na hatakula bamia.
Atataka kanziri, dini inakatalia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
11. Hataipenda achari, japo kuijaribia.
Atakataa hariri, suruwali kukuvalia.
Hutakuwa na khiyari, mwisho utamkimbia!
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
12. Maboi utaajiri, chipsi kumkaangia.
Utaweka askari, nyumba wa kumlindia.
Kila siku shayiri, hali bada asilia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
13. Unyumbani alasiri, raha itakuishia.
Kumpendeza kwa ari, yote utamfanyia.
Mwishowe wafikiri, jamani nenda jua!
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
14. Ajuta leo Ashuri, uzunguni kuolea.
Mno akabili hari, nyumbani yaloingia.
Hata babuye Omari, ya jikoni yamtishia!
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
15. Katoe fedha mahari, Bakari nakuusia.
Kwenu oa mwanamwari, harusi fanya aslia.
Mgenu epuka shari, kwenu asiye jadia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
16. Utahisi vizuri, ukioa Swahilia.
Atafukiza buhuri, mke marashi kutia.
Atajipaka uturi, mengi ya kufurahia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
17. Atavalia hariri, na libasi za darzia.
Ndipo utapoa hari, na roho itatulua.
Utaipenda mandhari, mazuri kukupikia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
18. Maakuli ya bizari, mke ataandalia.
Na chai ya zaatari, maandazi na bajia.
Utatafuna kidari, kwa mapishi kukolea.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
19. Na wewe utanawari, heshima itaingia.
Utafanya na nadhari, ndugu watafurahia.
Yote yatakuwa shwari, maisha yatatulua.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.
20. Kaditamati ya akhiri, mwisho nimefikia.
Kwaheri ndugu Bakari, haya yote zingatia.
Nakutakia ya kheri, Mola Atakujalia.
Mke wa ng'ambo achia, nakuusia Bakari.

*Hassan Adam (HAU), Cologne, Ujerumani
Julai, 2002.*